



TANGAZO LA MAENEO YA KUPANGA KWA AJILI YA KUTOLEA HUDUMA KWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) kinapenda kuutangazia umma kuwa kimetenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

Na.	ENEO	KAMPASI/MAHALI	HUDUMA INAYOTAKIWA
1.	Hill Park Supermarket (Mkataba wa muda mfupi wa miezi sita)	Hill Park	Mahitaji Mbalimbali
2.	Chumba Namba 1, Hall IV - Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Saluni ya Kiume

Kwa tangazo hili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawaalika wale wote wenye nia na wanaopenda kutoa huduma hizo kama zilivyoainishwa katika jedwali hapo juu kuomba kutoa huduma. Waombaji wafike Kurugenzi ya Mipango, Mendeleo na Uwekezaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Ofisi Namba 303 Jengo la Utawala (Cranford Pratt Building) kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi. Waombaji watalipa Shilingi elfu kumi tu (TZS 10,000/=) kupitia 'Namba ya Kumbukumbu' ambayo inapatikana Ofisi Namba 225 kwa Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Mwisho wa kuchukua fomu na kurudisha ni siku ishirini na moja (21) kutoka siku ya kwanza ya tangazo hili.

Tarehe **15 Septemba 2022** itakuwa ni siku ya kutembelea maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutolea huduma hizo ambapo saa 4:00 asubuhi tutakutana katika Kampasi Mwl. J. K. Nyerere Mlimani.

Baada ya mchakato wa kupata watoa huduma kukamilika, waombaji wote wataarifiwa juu ya matokeo hayo kwa njia ya barua.

Imetolewa na
NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – MIPANGO, FEDHA NA UTAWALA
31.08.2022